

## **NI WEWE**

Wewe ndiye yule mtu muhimu, sahihi na mzuri unayemtafuta siku zote.

Ninaujasiri wa kukwambia hivi, kwa sababu ni ukweli kwamba nguvu na uwezo wa mbegu hauko mbali na mbegu ila ndani yake, ni jambo la muda tu.

Unaweza kuamini kwamba miti mikubwa na mizuri inayopendeza machoni, yote ilitoka kwenye mbegu ndogo ambayo hata haijai kwenye kiganja? Ndio! Huu ndio ukweli, unaweza kuzani kwamba mbegu haijitoshelezi lakini sivyo uhalisia ulivyo.

Najua unamtafuta mtu sahihi, mzuri na wa muhimu ndio ujenge nae mahusiano, lakini mimi ninakwambia mtu huyo hayuko kwingine popote duniani ila yumo ndani yako.

Ukweli ni kwamba tumeacha na tumejisahau kuwa na vitu tunavyopaswa kuwa navyo na badala yake tunavitafuta kwa wengine.

Badala ya wewe kujipenda unatafuta mtu wa kukupenda, upendo ni wajibu wako.

Wewe unajitosheleza kwa kila kitu, hauhitaji mtu wa kukupa kitu ila wa kushirikishana vitu, kwa sababu wote mnajitosheleza.

Unahitaji kujitazama kwa upya ili uone uzuri, uwezo na nguvu zilizo ndani yako kuwa yule unayetamani kuwa. Tazama zaidi ya madhaifu yako ili uone uzuri wako.

Wengi watakwambia haujitoshelezi, lakini si kweli, kama ni kweli basi sisi sote ni wagonjwa, je ni nani wa kumsaidia mwenzie? Hapana! Wale wanaolitambua hili kuwa wanajitosheleza ndio watu muhimu zaidi wanaowasaidia wengine kutoka kwenye dimbwi hilo la giza.

Ukijiona kuwa hujitoshelezi ni hakika maisha yako yote utakuwa ni mtumwa na utakosa furaha maisha yako yote. Utatafuta vitu vya kukufanya ujitosheleze navyo havita kusaidia utaishia kujuta na kuharibikiwa.

Wewe unafikiri kwanini watu wanashawishika kununua vitu vya bei ghari? Moja ya sababu ni hii wanajihisi hawajitoshelezi. Watu wanatumia vipodozi vikali kwa sababu wanaona muonekano wao haujitoshelezi.

Hii ndiyo sera ya wafanya biashara, wanakuonyesha kuwa haujitoshelezi ili ununue bidhaa zao, lakini si kweli kwamba haujitoshelezi.

Kama wewe unaona haujitoshelezi ni kitu gani kitakutosheleza au ni nani atajitoa akutosheleze wewe?

Kuna mtu aliwahi kuniambia maneno haya wakati fulani nilipokuwa na huzuni “ Emma hebu jihudumie kama vile

unavyoweza kumuhudumia yule mtu unaye mpenda zaidi kwenye moyo wako”.

Niligundua hiki kitu kuwa hutatamani kuona machozi ya huzuni kwa yule umpendaye, hutatamani ateseke wala aumie mbele yako, hivyo kama ndivyo na mimi sitakiwi kuruhusu huzuni initawale kwa sababu napaswa kujipenda.

Baada ya hapo nilipata kitu cha kuinua maisha yangu, nilijitunza na kujipenda mno sikuruhusu moyo wangu uteseke na kitu chochote kwa muda mrefu, kwasababu niliona ninajitosheleza kujipenda na kujifanyia chochote ninachohitaji.

Mwisho niligundua kuwa mimi ndiye yule nliyekuwa namtafuta, nilikuwa namtafuta mtu wa kunifariji kumbe ninaweza nikaamua kuwa na furaha mwenyewe tu na inawezekana.

Kumbe unaweza kuruhusu ujione haujitoshelezi na unaweza kuruhusu ujione unajitosheleza ni vile ulivyochagua kuona, lakini hivi vyote haviui uhalisia wa kuwa unajitosheleza.

Mungu alipokuumba alikuumba na kila kitu unachopaswa kuwa nacho , hivyo ni wewe uamuzi wako wa kuvitumia hivyo vitu alivyokupa Mungu.

Furaha na huzuni zote zipo kwa ajili yako, sasa inategemea wewe umechagua kipi ukitunze ndani yako. Habari njema ni kuwa furaha ni uamuzi wako na huzuni ni uamuzi wako pia.